# MUHTASARI WA PATO LA TAIFA

## ROBO YA PILI (APRILI - JUNI) 2023

### BEI ZA MWAKA WA KIZIO 2015

TAKWIMU KWA MAENDELEO

Ofisi ya Taifa ya Takwimu
Wizara ya Fedha
Juni 2023

## Yaliyomo


1.0 Utangulizi ........ 1
1.1 Uchumi wa Dunia ........ 1
1.2 Nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara ........ 1
1.3 Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ........ 1
1.4 Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ........ 2
1.5 Ukuaji wa Uchumi Nchini Tanzania ........ 3
1.5.1 Pato la Taifa, Robo ya Pili ya Mwaka 2023 ........ 4
1.5.2 Mchango katika Pato la Taifa Robo ya Pili, Mwaka 2023 ........ 4
1.5.3 Ukuaji wa Shughuli za Uchumi Kipindi cha Robo ya Pili, Mwaka 2023 ........ 5
1.5.4 Mchango katika Kiwango cha Ukuaji Robo ya Pili, Mwaka 2023 ........ 6
2.0 Viwango vya Ukuaji kwa Shughuli za Kiuchumi ........ 6
2.1 Kilimo, Misitu na Uvuvi ........ 6
2.1.1 Mazao ........ 6
2.1.2 Mifugo ........ 6
2.1.3 Misitu ........ 7
2.1.4 Uvuvi ........ 7
2.2 Uchimbaji Madini na Mawe ........ 7
2.3 Uzalishaji Viwandani ........ 8
2.4 Umeme ........ 8
2.5 Usambazaji Maji ........ 9
2.6 Ujenzi ........ 10
2.7 Biashara na Matengenezo ........ 10
2.8 Uchukuzi na Uhifadhi wa Mizigo ........ 10
2.9 Malazi na Huduma za Chakula ........ 11
2.10 Habari na Mawasiliano ........ 11
2.11 Fedha na Bima ........ 11
2.12 Upangishaji Majengo ........ 12
2.13 Shughuli za Kitaalam, Ufundi na Sayansi ........ 12
2.14 Huduma Zinazohusiana na Utawala ........ 13
2.15 Utawala na Ulinzi ........ 13
2.16 Elimu ........ 13
2.17 Afya ........ 14
2.18 Huduma Nyingine za Jamii ........ 14
3.0 Hitimisho ........ 15

## Majedwali

Jedwali Na. 1: Uzalishaji wa Madini Robo ya Pili, Mwaka 2019 – 2023........................................8

## Orodha ya Vielelezo

Kielelezo Na. 1: Ukuaji wa Uchumi kwa Baadhi ya Nchi za SADC, Robo ya pili 2022 na 2023 ... 2
Kielelezo Na 2: Ukuaji wa Uchumi kwa Baadhi ya Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Robo ya Pili Mwaka 2019 – 2023 ... 3
Kielelezo Na. 3: Kiwango cha Ukuaji wa Pato la Taifa, Robo ya Pili Mwaka 2019 – 2023 ... 4
Kielelezo Na. 4: Mchango katika Pato la Taifa kwa Bei za Miaka Husika ... 5
Kielelezo Na. 5: Viwango vya Ukuaji wa Shughuli za Uchumi, Robo ya Pili, Mwaka 2023 ... 5
Kielelezo Na. 6: Uzalishaji Maji (Mita za Ujazi Milioni) Robo ya Pili, Mwaka 2019 – 2023 ... 9
Kielelezo Na. 7: Thamani ya Mikopo na Amana, Robo ya Pili, Mwaka 2019 – 2023 ... 12

## 1.0 Utangulizi

Pato la Taifa kwa robo mwaka ni kiashiria chenye taarifa za kina za mwenendo wa shughuli za uchumi. Kiashiria hiki hutumika katika kutathmini mwenendo wa shuguli za kiuchumi kwa vipindi vifupi vifupi kwa lengo la kutunga na kutathmini sera za kiuchumi kwa wakati muafaka katika nchi.

## 1.1 Uchumi wa Dunia

Kwa mujibu wa ripoti ya hali ya uchumi wa dunia iliyotolewa na Shirika la Fedha Duniani (IMF) mwezi Julai 2023, uchumi wa dunia ulikadiriwa kukua kwa kiwango cha asilimia 3.0 mwaka 2023 ikiwa ni ongezeko kwa kiwango cha pointi za asilimia 0.2 ikilinganishwa na kiwango kilichokadiriwa kwenye Maoteo yaliyofanyika mwezi Aprili Mwaka 2023 ambayo yalikadiria ukuaji wa asilimia 2.8.

Kuongezeka kwa kasi ya ukuaji kumetokana na sababu mbalimbali ikiwemo: kuimarika kwa uzalishaji na usambazaji wa bidhaa, na gharama za usafirishaji kurejea katika viwango vya kawaida kama ilivyokuwa kabla ya janga la Uviko-19. Aidha, uchumi wa dunia katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2023 umeonesha kuimarika zaidi. Vilevile, sera za kubana mikopo zinazoendeshwa na Benki Kuu za nchi zilizoendelea zimechangia kupunguza kiasi cha fedha kwa ajili ya kukopesha nchi masikini hivyo kupunguza uwezo wa uwekezaji. Hii imechangia ukuaji wa uchumi katika nchi hizo kutofikia kiwango kilichokuwepo kabla ya janga la UVIKO-19.

## 1.2 Nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara

Ukuaji wa uchumi wa nchi zilizo kusini mwa Jangwa la Sahara ulikadiriwa kuongezeka kwa kiwango cha asilimia 3.5 mwaka 2023 ambacho ni sawa na upungufu kwa asilimia za pointi 0.1 ukilinganishwa na makadirio yaliyofanyika kwenye Maoteo ya mwezi Aprili 2023 yaliyokadiria kiwango cha ukuaji wa asilimia 3.6. Uchumi wa nchi ya Afrika Kusini ulikadiriwa kukua kwa kiwango cha asilimia 0.3 mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia za pointi 0.2 kutoka kadirio la asilimia 0.1 lililokuwa limekadiriwa kwenye ripoti ya Aprili 2023.Aidha, katika kipindi hicho uchumi wa Nigeria umekadiriwa kuongezeka kwa asilimia 3.2 kama ulivyokadiriwa kwenye Maoteo ya mwezi Aprili 2023.


## 1.3 Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika

Kwa mujibu wa ripoti ya makadirio ya ukuaji wa uchumi mwezi Julai 2023 inayotolewa na Shirika la Fedha Duniani (IMF), ukuaji wa uchumi katika nchi za

Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika unatarajiwa kukua kwa asilimia 3.5 mwaka 2023 ikiwa ni pungufu kwa pointi za asilimia 0.1 ikilinganishwa na maoteo yaliyofanyika mwezi Aprili 2023.

Tathmini ya ukuaji wa uchumi kwa baadhi ya nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika unaonesha kuwa, uchumi wa nchi ya Afrika kusini umeongezeka kwa kiwango cha asilimia 1.6 katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2023 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 0.2 kipindi kama hicho mwaka 2022. Uchumi wa Namibia uliongezeka kwa kiwango cha asilimia 3.7 katika robo ya pili mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 8.5 kipindi kama hicho mwaka 2022. Uchumi wa Botswana ulikua kwa kiwango cha asilimia 3.4 katika robo ya pili mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 5.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Aidha, uchumi wa Tanzania umeongezeka kwa kiwango cha asilimia 5.2 katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2023 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 4.7 kipindi kama hicho mwaka 2022.

**Kielelezo Na. 1: Ukuaji wa Uchumi kwa Baadhi ya Nchi za SADC, Robo ya pili 2022 na 2023**





**Chanzo: Tovuti za Ofisi za Takwimu za Nchi Husika, 2023**

## 1.4 Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki

Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ambazo zimetoa taarifa za mwenendo wa shughuli za uchumi katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2023 zimeonesha kuendelea kuimarika kwa ukuaji chanya wa uchumi. Kiwango cha ukuaji wa uchumi kwa nchi ya Rwanda kimeongezeka kwa asilimia 6.3 ikilinganishwa na asilimia 7.5 kipindi kama hicho mwaka 2022. Aidha, uchumi wa Uganda umekua kwa kiwango cha asilimia 6.8 katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2023 ikilinganishwa na

ukuaji wa asilimia 5.6 katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Vilevile, uchumi wa Tanzania umekua kwa kiwango cha asilimia 5.2 ukilinganishwa na asilimia 4.7 katika robo ya pili mwaka 2022. Taarifa za mwenendo wa ukuaji wa uchumi kwa nchi nyingine wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika kipindi cha mwezi Aprili hadi Juni 2023 hazijapatikana.

**Kielelezo Na 2: Ukuaji wa Uchumi kwa Baadhi ya Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Robo ya Pili Mwaka 2019 – 2023**




**Chanzo: Tovuti za Ofisi za Takwimu za Nchi Husika, 2023**

## 1.5 Ukuaji wa Uchumi Nchini Tanzania


Utayarishaji wa Takwimu za Pato la Taifa katika kipindi cha robo ya pili (Aprili - Juni) 2023 umetumia taarifa zilizokusanywa kutoka katika shughuli zote za kiuchumi zilizofanyika nchini. Aidha, utayarishaji umezingatia Mwongozo wa Kimataifa wa Kutayarisha Takwimu za Pato la Taifa unaojulikana kama *System of National Accounts 2008 (2008 SNA)*. Taarifa hii inahusu Pato la Taifa kwa Tanzania Bara kwa bei za mwaka husika na Pato la Taifa kwa bei za mwaka 2015.

Ofisi ya Taifa ya Takwimu inaendelea kutekeleza Sera ya Mapitio ya Takwimu za Pato la Taifa iliyoanza kutumika mwaka 2019. Sera hii inapendekeza kuchapisha matokeo ambayo yanaweza kufanyiwa mapitio kutokana na kupatikana kwa takwimu mpya au zilizofanyiwa mapitio za kila robo mwaka na za kila mwaka. Kutokana na mapitio ya Sera hii na maboresho yaliyofanyika kwenye takwimu za urari wa biashara zinazotolewa na Benki Kuu ya Tanzania, takwimu za Pato la Taifa za mwaka 2017 - 2022 zimefanyiwa mapitio.

### 1.5.1 Pato la Taifa, Robo ya Pili ya Mwaka 2023

Katika kipindi cha robo ya Pili ya mwaka 2023, Pato la Taifa kwa bei za mwaka husika (*current prices*) liliongezeka hadi Shilingi trilioni 47.6 kutoka Shilingi trilioni 42.6 kipindi kama hicho mwaka 2022. Aidha, Pato la Taifa kwa bei za mwaka 2015 (*constant prices*) liliongezeka hadi Shilingi trilioni 36.7 katika kipindi cha robo ya Pili mwaka 2023 kutoka Shilingi trilioni 34.9 katika kipindi kama hicho mwaka 2022, ikiwa ni sawa na ongezeko halisi la asilimia 5.2.

**Kielelezo Na. 3: Kiwango cha Ukuaji wa Pato la Taifa, Robo ya Pili Mwaka 2019 – 2023**





**Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu, 2023**

### 1.5.2 Mchango katika Pato la Taifa Robo ya Pili, Mwaka 2023

Mchanganuo wa mchango wa makundi makuu ya shughuli za kiuchumi katika Pato la Taifa katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2023 unaonesha kuwa Shughuli za Huduma zilikuwa na mchango mkubwa zaidi wa asilimia 39.2, zikifuatiwa na Shughuli za Msingi asilimia (38.6), na Shughuli za Kati asilimia (22.2). Mchango wa makundi makuu ya shughuli kuu za kiuchumi katika Pato la Taifa umekokotolewa kwa bei za mwaka husika kabla ya kujumuisha kodi.

**Kielelezo Na. 4: Mchango katika Pato la Taifa kwa Bei za Miaka Husika**





**Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu, 2023**

### 1.5.3 Ukuaji wa Shughuli za Uchumi Kipindi cha Robo ya Pili, Mwaka 2023

Katika kipindi cha Aprili hadi Juni 2023, shughuli ya kiuchumi ya Fedha na Bima iliongoza kwa ukuaji wa (asilimia 15.6), ikifuatiwa na uzalishaji na usambazaji umeme (asilima 12.4), huduma nyingine za jamii zinazojumuisha sanaa na burudani na shughuli za kaya katika kuajiri (asilimia 11.5), Uchukuzi na uhifadhi mzigo (asilimia 7.6), huduma ya chakula na malazi asilimia (7.2), biashara na matengenezo (asilimia 6.4), uchimbaji wa madini na mawe (asilimia 6.3), habari na mawasiliano (asilimia 6.2) na uzalishaji viwandani (asilimia 6.1).

**Kielelezo Na. 5: Viwango vya Ukuaji wa Shughuli za Uchumi, Robo ya Pili, Mwaka 2023**




**Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu, 2023**

### 1.5.4 Mchango katika Kiwango cha Ukuaji Robo ya Pili, Mwaka 2023

Shughuli zote za uchumi zilizofanyika katika kipindi cha Aprili hadi Juni 2023 zilichangia katika ukuaji wa uchumi kwa viwango tofauti. Katika kipindi hicho, shughuli za kiuchumi zilizochangia zaidi katika ukuaji zilikuwa ni pamoja na: kilimo (asilimia 11.9), usafirishaji na uhifadhi wa mizigo (asilimia 11.6); fedha na bima (asilimia 10.5), biashara na matengenezo (asilimia 10.3); uzalishaji viwandani (asilimia 9.2), na ujenzi (asilimia 6.9).

## 2.0 Viwango vya Ukuaji kwa Shughuli za Kiuchumi

### 2.1 Kilimo, Misitu na Uvuvi

Shughuli hii inahusika na uvunaji wa rasilimali za asili za mboga za majani na wanyama. Shughuli hizi zinazojumuisha mazao ya kupandwa, ufugaji na uzalishaji wa wanyama, uvunaji wa miti na mimea mingine, wanyama au bidhaa za wanyama kutoka katika mashamba ya ufugaji au mazingira ya asili.

#### 2.1.1 Mazao

Mazao makuu yaliyojumuishwa ni pamoja na mahindi, mpunga, ulezi/mtama, nafaka nyingine, mihogo, viazi mviringo, viazi vitamu, maharagwe, mikunde, mbegu za mafuta, mboga mboga, ndizi, matunda mengine, karanga, kahawa, pamba, chai, tumbaku na mazao mengine ya chakula na biashara.

Shughuli ya kilimo cha mazao iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 1.2 katika robo ya pili ya mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 3.0 kipindi kama hicho mwaka 2022. Ukuaji huo ulichangiwa na kuongezeka kwa uzalishaji uliotokana na matumizi ya teknolojia na pembejeo bora; pamoja kuimarika kwa huduma za ugani.

#### 2.1.2 Mifugo

Shughuli hii inahusika na ufugaji ng'ombe wa asili na wa kisasa; mbuzi, kondoo, punda, farasi, nguruwe, sungura, kuku wa kienyeji na kisasa; na ndege wa aina nyingine.

Katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2023, uzalishaji wa mifugo uliongezeka kwa kiwango cha asilimia 5.1 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.0 kipindi kama hicho mwaka 2022. Ukuaji huo ulichangiwa na kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa za mifugo, ukuaji wa miji pamoja na kuongezeka kwa uelewa wa wananchi juu ya umuhimu wa kutumia lishe bora kutokana na mazao ya Mifugo.

### 2.1.3 Misitu

Shughuli hii inahusisha uzalishaji na uvunaji wa mazao ya misitu kama vile magogo, mkaa, kuni, matawi ya miti, na bidhaa nyingine zisizo za miti kama vile asali na nta.

Shughuli ya misitu ilikua kwa kiwango cha asilimia 3.9 katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 2.4 kipindi kama hicho mwaka 2022. Ukuaji huo ulitokana na kuongezeka kwa usimamizi wa rasilimali za misitu na juhudi za Serikali katika kuhakikisha uvunaji endelevu wa bidhaa za misitu.

### 2.1.4 Uvuvi

Shughuli ya uvuvi inahusika na uvunaji wa rasilimali za uvuvi katika maji ya bahari na vyanzo vingine vya maji baridi.

Shughuli ya uvuvi iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 1.0 katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2023 ikilinganishwa na ukuaji hasi wa asilimia 1.0 katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Kuongezeka kwa kasi ya ukuaji wa shughuli ya uvuvi ulichangiwa na juhudi za Serikali katika kusimamia uvunaji wa mazao ya uvuvi katika kipindi hicho.

## 2.2 Uchimbaji Madini na Mawe

Shughuli ya uchimbaji wa madini na mawe inahusisha uchimbaji au ukusanyaji wa madini katika hali zake za yabisi kama vile makaa ya mawe, vimiminika (mfano petroli) au gesi (mfano gesi asilia). Uchimbaji wa madini na mawe hufanyika chini ya ardhi, ukusanyaji juu ya ardhi au kwenye visima. Uchimbaji wa madini na mawe pia unajumuisha shughuli za ziada zinazolenga kutayarisha madini kwa ajili ya kuuzwa, kwa mfano, kusaga, kusafisha na kukausha. Shughuli hizi mara nyingi zinafanywa na vitengo ambavyo vinavuna rasilimali za madini / au nyingine zilizopo karibu na migodi.

Shughuli ya uchimbaji wa madini na mawe imegawanyika katika maeneo makuu manne ambayo ni:

i. Madini ya makaa ya mawe;
ii. Petroli na gesi asilia;
iii. Uchimbaji wa madini ya chuma; na
iv. Madini ya kokoto na mawe.

Katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2023, shughuli ya uchimbaji wa madini na mawe iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 6.3 ikilinganishwa na asilimia 5.8

kipindi kama hicho mwaka 2022. Ukuaji wa shughuli hii ulitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa madini ya Tanzanite, makaa ya mawe, chumvi, fedha na madini ya pozzolana ambayo ni mali ghafi ya kutengeneza saruji. (***Jedwali Na. 1***)

**Jedwali Na. 1: Uzalishaji wa Madini Robo ya Pili, Mwaka 2019 – 2023**

| Madini | Kipimo | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Fedha | Tani | 3,358 | 2,768 | 1,685 | 3,444 | 4,094 |
| Makaa ya Mawe | Tani | 181,236 | 148,869 | 247,770 | 537,563 | 623,759 |
| Chumvi | Tani | 30,268 | 9,311 | 15,949 | 32,161 | 47,258 |
| Gesi asilia | Mscf | 14,087 | 12,146 | 12,385 | 13,565 | 20,106 |

**Chanzo: Wizara ya Madini 2023**

## 2.3 Uzalishaji Viwandani

Shughuli ya uzalishaji viwandani inahusisha uchakataji wa bidhaa kutoka katika hali yake ya kawaida na kuzalisha bidhaa za aina nyingine ambazo zinaweza kutumika moja kwa moja na mlaji wa mwisho au kutumika kuzalisha bidhaa nyingine. Bidhaa zinazoweza kuchakatwa ni pamoja na bidhaa za kilimo, misitu, uvuvi, madini na bidhaa nyingine za viwandani.

Kiwango cha ukuaji wa shughuli ya uzalishaji viwandani kiliongezeka hadi asilimia 6.1 katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2023 kutoka asilimia 4.7 kipindi kama hicho mwaka 2022. Ukuaji huu ulichangiwa na ongezeko la uzalishaji wa bidhaa za viwandani.

## 2.4 Umeme

Shughuli hii inahusika na uzalishaji na usambazaji wa umeme na gesi asilia, kupitia miundombinu ya kudumu ya waya na mabomba. Uzalishaji wa umeme ni kutoka katika vyanzo vya maji, mafuta na gesi. Shughuli hii inahusika na usambazaji na ugawaji wa umeme. Vyanzo vikuu vya takwimu za uzalishaji wa umeme ni kutoka katika makampuni ya uzalishaji wa umeme.

Ukuaji wa shughuli ya uzalishaji wa nishati ya umeme hutegemea kiasi cha umeme kilichozalishwa na kusambazwa kwa wateja mbalimbali. Katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2023, kiasi cha umeme kilichosambazwa kiliongezeka hadi saa za kilowati milioni 2,155 kutoka saa za kilowati milioni 1,918 kipindi kama hicho mwaka 2022.

Shughuli ya uzalishaji umeme iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 12.4 katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 8.7 kipindi kama hicho mwaka 2022.


## 2.5 Usambazaji Maji

Shughuli hii inahusika na kukusanya na kusafisha maji kwa ajili ya ugavi, kusafisha maji ya bahari kwa kuondoa chumvi ili kuzalisha maji ya kutumia kama bidhaa kuu na kukusanya maji moja kwa moja kutoka katika visima kwa ajili ya matumizi ya makampuni ya maji au matumizi binafsi katika kilimo au kaya. Vilevile, shughuli hii inahusika na ukusanyaji wa maji taka.

Kiashiria cha kuongezeka kwa kiwango cha ukuaji wa shughuli ya usambazaji maji ni kiasi cha maji kilichozalishwa. Katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2023, kiasi cha maji kilichozalishwa kiliongezeka hadi mita za ujazo milioni 93.3 kutoka mita za ujazo milioni 90.2 zilizozalishwa kipindi kama hicho mwaka 2022.

Kiwango cha ukuaji wa shughuli ya usambazaji maji kilikuwa asilimia 3.3 katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 9.5 kipindi kama hicho mwaka 2022.

**Kielelezo Na. 6: Uzalishaji Maji (Mita za Ujazi Milioni) Robo ya Pili, Mwaka 2019 – 2023**




**Chanzo: Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji, 2023**

## 2.6 Ujenzi

Shughuli hii inajumuisha ujenzi wa aina zote na shughuli maalum za ujenzi kwa ajili ya majengo na kazi za uhandisi. Shughuli hii inajumuisha pia ujenzi mpya, ukarabati, kufanya mabadiliko makubwa kwenye majengo na ujenzi wa miundombinu.

Shughuli za ujenzi zinajumuisha, ujenzi wa nyumba za kuishi na nyumba za makazi, ujenzi wa majengo ya biashara au ofisi, maduka na majengo mengine ya umma na miundombinu ya mashambani. Shughuli hii  pia unajumuisha ujenzi wa barabara, madaraja, reli, viwanja vya ndege, bandari na miundombinu ya maji, mifumo ya umwagiliaji, mifumo ya majitaka, miundombinu ya viwanda, mabomba, mifumo ya umeme na vituo vya michezo.

Katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2023, shughuli ya ujenzi iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 2.3 ikilinganishwa na asilimia 4.0 kipindi kama hicho mwaka 2022. Tathmini ya ukuaji wa shughuli ya ujenzi hutumia viashiria vya uzalishaji wa bidhaa za ndani ya nchi zinazotumika katika ujenzi. Ukuaji wa shughuli hii ulitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa za ujenzi ikiwa ni ni pamoja na bidhaa za chuma.

## 2.7 Biashara na Matengenezo

Shughuli hii inajumuisha uuzaji wa jumla na rejareja (uuzaji wa bidhaa bila ya kufanya mabadiliko) wa aina yoyote ya bidhaa, pamoja na utoaji wa huduma kwa ajili ya uuzaji wa bidhaa. Pia inahusisha ukarabati wa magari na usimikaji wa mitambo na ukarabati wa bidhaa binafsi za nyumbani. Shughuli kuu ni kununua na kuuza bidhaa.

Ukuaji wa shughuli ya biashara na matengenezo iliongezeka kwa asilimia 6.4 katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2023 kutoka asilimia 4.9 kipindi kama hicho mwaka 2022. Ukuaji wa shughuli hii ulichangiwa na kuongezeka kwa bidhaa zilizouzwa ikiwa ni pamoja na bidhaa zilizozalishwa viwandani na zilizoagizwa kutoka nje ya nchi.

## 2.8 Uchukuzi na Uhifadhi wa Mizigo

Shughuli hii inahusisha utoaji wa huduma ya usafiri wa abiria au/na mizigo, ikiwa ni kwa ratiba maalum au isiyokuwa na ratiba, kwa njia ya reli, bomba, barabara, maji au anga na shughuli zinazohusiana ikiwa ni pamoja na utunzaji wa mizigo na

uhifadhi. Shughuli hii pia inajumuisha kukodisha vifaa vya usafiri na madereva na shughuli za posta na usafirishaji wa vifurushi.

Kasi ya ukuaji wa shughuli ya uchukuzi na uhifadhi wa mizigo iliongezeka hadi kiwango cha asilimia 7.6 katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2023 kutoka asilimia 4.1 kipindi kama hicho mwaka 2022. Ukuaji huu umetokana na kuongezeka kwa idadi ya abiria na mizigo iliyosafirishwa kwa njia ya barabara katika kipindi hicho.

### 2.9 Malazi na Huduma za Chakula

Shughuli hii inajumuisha utoaji huduma ya makazi ya muda mfupi kwa wageni na wasafiri wengine na utoaji wa huduma ya chakula na vinywaji kwa mlaji wa mwisho.

Shughuli ya malazi na huduma za chakula iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 7.2 katika robo ya pili ya mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 13.0 kipindi kama hicho mwaka 2022. Kasi ya ukuaji wa shughuli ya malazi na huduma za chakula katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2023 ilichangiwa na kuongezeka kwa idadi ya watalii walioingia nchini ambao walifikia 350,245 kutoka watalii 286,025 walioingia nchini kipindi kama hicho mwaka 2022.

### 2.10 Habari na Mawasiliano

Shughuli hii inahusika na uchapishaji, upigaji picha za kawaida, picha za video na uzalishaji wa programu za televisheni, kurekodi sauti na kuchapisha muziki, shughuli za programu na utangazaji kwa mfano utangazaji wa redio na televisheni, mawasiliano ya simu, programu za kompyuta, ushauri na shughuli zinazohusiana na shughuli za huduma za habari kama vile uchakataji wa taarifa.


Kiwango cha ukuaji wa shughuli ya habari na mawasiliano kiliongezeka kwa asilimia 6.2 katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 6.7 kipindi kama hicho mwaka 2022. Kasi ya ukuaji ilitokana na huduma za ujumbe mfupi uliotumwa na idadi ya wateja waliopata huduma za fedha kupitia mitandao ya simu pamoja na huduma za utangazaji na huduma za inteneti kwa ujumla.

### 2.11 Fedha na Bima

Shughuli hii inahusika na utoaji wa huduma za fedha, bima, pensheni ya hiari, na huduma nyingine za fedha.

Huduma ya fedha na bima iliongezeka hadi kiwango cha asilimia 15.6 katika robo ya pili ya mwaka 2023 kutoka asilimia 9.0 katika robo ya pili ya mwaka 2022. Ukuaji wa shughuli ya fedha na bima ilichangiwa na kuongezeka kwa asilimia 20.8 kwa amana za wateja kutoka shilingi trilioni 28.0 mwaka 2022 hadi shilingi trilioni 33.7 mwaka 2023; kuongezeka kwa asilimia 22.4 kwa mikopo kutoka shilingi trilioni 24.1 mwaka 2022 hadi shilingi trilioni 29.6 mwaka 2023.

**Kielelezo Na. 7: Thamani ya Mikopo na Amana, Robo ya Pili, Mwaka 2019 – 2023**




**Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania, 2023**

## 2.12 Upangishaji Majengo

Shughuli hii inahusika na utoaji wa huduma za kuuza au kununua majengo, kukodisha mali, majengo na pia kutoa huduma nyingine za mali isiyohamishika ikiwa ni pamoja na kupima mali isiyohamishika kama vile viwanja.

Kiwango cha ukuaji wa shughuli ya upangishaji majengo kiliongezeka kwa asilimia 4.2 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 4.4 kipindi kama hicho mwaka 2022. Ongezeko la mahitaji ya huduma za malazi hususan katika maeneo ya mjini lilichangia ukuaji wa shughuli hii ya uchumi.

## 2.13 Shughuli za Kitaalam, Ufundi na Sayansi

Shughuli hii inajumuisha shughuli maalum za kitalaam, kisayansi na kiufundi. Shughuli hizi zinahitaji kiwango cha juu cha mafunzo, pamoja na kupata ujuzi maalum unaotumika kutoa huduma kwa watumiaji. Shughuli hii inahusisha huduma

za kisheria na uhasibu; ushauri na usimamizi; usanifu na uhandisi; kupima na uchambuzi wa kitaalam; utafiti wa kisayansi na maendeleo; matangazo na utafiti wa masoko; utaalam wa aina nyingine wa kisayansi na kiufundi pamoja na shughuli za ugani.

Kasi ya ukuaji wa shughuli za kitaalam, kisanyansi na kiufundi iliongezeka kwa asilimia 4.7 katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 5.5 katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Huduma za kisheria na uhasibu zilichangia katika kiwango cha ukuaji uliofikiwa.

### 2.14 Huduma Zinazohusiana na Utawala

Shughuli hii inajumuisha huduma mbalimbali zinazosaidia kufanyika kwa biashara ambazo ni huduma za: kukodisha vifaa, ajira, uwakala wa kampuni za usafiri, kuongoza watalii, kuandaa malazi; na huduma nyingine zinazohusiana na usalama na uchunguzi; pamoja na huduma kwenye majengo na uboreshaji wa mazingira.

Kiwango cha ukuaji wa Huduma zinazohusiana na Utawala kiliongezeka hadi kiwango cha asilimia 5.8 katika robo ya pili ya mwaka 2023 kutoka asilimia 5.2 kipindi kama hicho mwaka 2022. Kuongezeka kwa huduma za uwakala wa usafiri wa watalii ulichangia zaidi ukuaji wa shughuli hiiya kiuchumi.

### 2.15 Utawala na Ulinzi

Shughuli ya Utawala na Ulinzi inahusika na kutunga na kutafsiri sheria, kukusanya kodi, ulinzi wa mipaka ya nchi, usalama wa raia na mali zao, huduma za uhamiaji, pamoja na uendeshaji wa Serikali kwa ujumla. Aidha, huduma za mifuko ya hifadhi ya jamii ya lazima imejumuishwa katika shughuli ya Utawala na Ulinzi.

Kasi ya ukuaji wa shughuli ya utawala na ulinzi iliongezeka hadi kiwango cha asilimia 5.0 katika robo ya pili ya mwaka 2023 kutoka asilima 4.8 kipindi kama hicho mwaka 2022. Kiwango cha ukuaji kilitokana na kuongezeka kwa matumizi ya fedha za Serikali katika mishahara, kulipa malimbikizo ya madai ya wafanyakazi na utekelezaji wa kazi za ulinzi na usalama pamoja na uendeshaji wa Serikali kwa ujumla.

### 2.16 Elimu

Shughuli hii inajumuisha utoaji wa elimu katika ngazi zote, kwa njia ya kuongea au maandishi au kwa njia ya redio na televisheni au njia nyingine za mawasiliano. Vilevile, inajumuisha elimu inayotolewa na taasisi mbalimbali katika mfumo wa kawaida wa shule katika ngazi tofauti pamoja na elimu ya watu wazima na elimu ya

kujifunza kusoma na kuandika. Shughuli hii inajumuisha elimu katika sekta ya umma na binafsi.

Shughuli ya elimu iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 5.5 katika robo ya pili ya mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 5.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Ukuaji wa shughuli hii umetokana na udahili wa wanafunzi katika ngazi zote za utoaji wa elimu za umma na binafsi ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa mishahara na matumizi ya Serikali katika utoaji wa elimu bila ada.

## 2.17 Afya

Shughuli hii inajumuisha utoaji wa huduma za afya na maendeleo ya jamii. Inajumuisha pia huduma za afya zinazotolewa na wataalam wa matibabu katika hospitali na vituo vingine, shughuli nyingine za huduma za makazi ambazo zinahusisha shughuli za huduma za afya kwa jamii bila ushirikishwaji wa wataalam wa huduma za afya.

Shughuli ya utoaji wa huduma za afya iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 4.9 katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 5.5 katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Ukuaji huu ulitokana na kuendelea kuboreshwa kwa huduma za utoaji wa huduma za afya kwa jamii katika ngazi zote za kutolea huduma katika vituo vya umma na binafsi na kuongezeka kwa ya mishahara ya watumishi wa umma.

## 2.18 Huduma Nyingine za Jamii

Shughuli hii inajumuisha shughuli za mashirika ya uanachama, ukarabati wa vifaa vya kieletroniki na bidhaa za kibinafsi za nyumbani na shughuli mbalimbali za huduma za binafsi ambazo hazijumuishwi kwenye shughuli nyingine. Pia inajumuisha shughuli ya sanaa na burudani na shughuli za kaya katika kuajiri.

Kasi ya ukuaji wa shughuli ya huduma nyingine za jamii zinazojumuisha sanaa na burudani na shughuli za kaya katika kuajiri iliongezeka hadi kiwango cha asilimia 11.5 katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2023 kutoka  asilimia 7.5 kipindi kama hicho mwaka 2022. Kuongezeka kwa watalii, idadi ya watu katika maeneo ya mjini na mahitaji ya huduma za jamii kulichangia ukuaji wa shughuli hii ya kiuchumi.

## 3.0 Hitimisho

Katika kipindi cha robo ya pili mwaka 2023, Pato halisi la Taifa liliongezeka kwa kiwango cha asilimia 5.2 ikilinganishwa na asilimia 4.7 kipindi kama hicho mwaka 2022. Shughuli zilizoongezeka kwa kiwango kikubwa zilikuwa ni pamoja na: fedha na bima ambayo iliongoza kwa ukuaji wa (asilimia 15.6); ikifuatiwa na uzalishaji na usambazaji umeme (asilima 12.4); huduma nyingine za jamii zinazojumuisha sanaa na burudani na shughuli za kaya katika kuajiri (asilimia 11.5); uchukuzi na uhifadhi mizigo (asilimia 7.6); huduma ya chakula na malazi asilimia (7.2); biashara na matengenezo (asilimia 6.4); uchimbaji wa madini na mawe (asilimia 6.3); habari na mawasiliano (asilimia 6.2) na uzalishaji viwandani (asilimia 6.1).

**Kiambatisho Na. 1: Pato la Taifa kwa Shughuli za kiuchumi kwa Bei za Mwaka 2015 – Sh. Milioni**

| Mwaka | Nusu Mwaka | kilimo | Madini na Mawe | Viwanda | Umeme | Maji safi na maji taka | Ujenzi | Biashara na Matengenezo | Malazi na Huduma ya Chakula | Uchukuzi na Uhifadhi Mizigo | Habari na Mawasiliano | Fedha na Bima |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2014 | | 23,952,077 | 3,687,273 | 6,919,794 | 815,297 | 381,760 | 9,253,082 | 8,444,243 | 1,397,782 | 6,577,706 | 1,560,064 | 3,764,113 |
| 2015 | | 25,234,560 | 4,055,619 | 7,411,672 | 798,801 | 390,758 | 10,446,797 | 8,747,862 | 1,421,916 | 6,929,895 | 1,681,098 | 4,189,021 |
| 2016 | | 26,436,338 | 4,356,709 | 8,213,364 | 869,262 | 417,899 | 11,960,720 | 9,260,703 | 1,480,052 | 7,324,856 | 1,718,548 | 4,235,515 |
| 2017 | | 27,999,287 | 4,588,624 | 8,889,818 | 877,667 | 444,660 | 13,765,005 | 9,820,627 | 1,525,619 | 7,815,845 | 1,824,472 | 4,115,393 |
| 2018 | | 29,504,246 | 4,659,195 | 9,623,501 | 928,174 | 477,510 | 15,655,747 | 10,396,754 | 1,604,391 | 8,736,561 | 1,989,716 | 4,094,972 |
| 2019 | | 30,802,708 | 5,485,112 | 10,184,558 | 994,879 | 510,411 | 17,802,021 | 10,965,088 | 1,645,950 | 9,493,191 | 2,133,313 | 4,281,167 |
| 2020 | | 32,323,885 | 5,887,452 | 10,646,279 | 1,049,610 | 540,159 | 19,421,672 | 11,196,820 | 1,419,654 | 10,293,276 | 2,313,029 | 4,412,967 |
| 2021 | | 33,587,556 | 6,442,881 | 11,155,762 | 1,154,204 | 575,213 | 20,249,939 | 11,590,506 | 1,514,711 | 10,658,344 | 2,524,564 | 4,629,490 |
| 2022 | | 34,711,277 | 7,146,141 | 11,624,144 | 1,242,132 | 606,754 | 21,131,032 | 12,046,448 | 1,651,099 | 11,061,950 | 2,712,411 | 5,024,141 |
| | | | | | | | | | | | | |
| 2012 | 1 | 5,972,854 | 845,470 | 1,528,195 | 151,473 | 86,422 | 1,816,993 | 1,877,418 | 321,003 | 1,208,445 | 281,981 | 849,590 |
| | 2 | 5,182,996 | 825,383 | 1,544,666 | 164,427 | 89,319 | 1,808,760 | 1,855,404 | 320,427 | 1,456,176 | 303,507 | 844,631 |
| | 3 | 4,092,001 | 833,592 | 1,499,895 | 172,946 | 92,526 | 2,012,312 | 1,725,714 | 358,248 | 1,489,645 | 327,526 | 886,247 |
| | 4 | 6,559,178 | 810,297 | 1,494,233 | 180,223 | 90,094 | 1,940,197 | 1,912,875 | 344,245 | 1,556,199 | 353,733 | 863,692 |
| 2013 | 1 | 5,994,220 | 748,412 | 1,459,422 | 167,460 | 87,306 | 2,146,785 | 1,828,162 | 332,454 | 1,519,508 | 312,238 | 811,387 |
| | 2 | 5,376,452 | 850,463 | 1,547,040 | 177,004 | 90,069 | 2,111,891 | 1,884,307 | 324,659 | 1,501,581 | 343,060 | 836,571 |
| | 3 | 4,199,755 | 875,290 | 1,677,731 | 181,477 | 85,918 | 2,389,873 | 1,893,295 | 354,104 | 1,513,039 | 358,452 | 881,698 |
| | 4 | 6,837,765 | 990,556 | 1,608,322 | 197,667 | 104,598 | 2,374,804 | 2,076,522 | 344,987 | 1,516,849 | 400,366 | 876,284 |
| | | | | | | | | | | | | |
| 2014 | 1 | 6,335,448 | 937,448 | 1,621,405 | 201,849 | 87,893 | 2,182,230 | 2,054,479 | 346,623 | 1,625,429 | 342,909 | 912,095 |
| | 2 | 5,877,120 | 871,899 | 1,706,772 | 182,845 | 94,708 | 2,507,336 | 2,073,942 | 339,327 | 1,616,710 | 380,305 | 927,895 |
| | 3 | 4,450,294 | 929,381 | 1,788,128 | 213,998 | 97,099 | 2,228,708 | 2,035,245 | 361,470 | 1,686,150 | 414,058 | 960,721 |
| | 4 | 7,289,215 | 948,546 | 1,803,489 | 216,605 | 102,059 | 2,334,808 | 2,280,578 | 350,362 | 1,649,417 | 422,793 | 963,401 |
| | | | | | | | | | | | | |
| 2015 | 1 | 6,605,887 | 923,326 | 1,733,636 | 211,828 | 96,862 | 2,438,046 | 2,093,973 | 346,778 | 1,654,599 | 386,446 | 995,846 |
| | 2 | 6,347,239 | 965,335 | 1,820,111 | 199,281 | 92,862 | 2,690,105 | 2,195,254 | 345,054 | 1,676,064 | 412,841 | 1,011,653 |
| | 3 | 4,656,388 | 960,427 | 1,939,664 | 192,215 | 99,585 | 2,601,253 | 2,162,776 | 372,080 | 1,764,202 | 441,478 | 1,076,143 |
| | 4 | 7,625,045 | 1,206,532 | 1,918,260 | 195,477 | 101,448 | 2,717,393 | 2,295,860 | 358,003 | 1,835,030 | 440,334 | 1,105,380 |
| | | | | | | | | | | | | |
| 2016 | 1 | 6,788,342 | 1,017,609 | 1,965,656 | 214,850 | 95,779 | 2,859,933 | 2,295,506 | 358,142 | 1,818,390 | 401,047 | 1,111,056 |
| | 2 | 6,853,095 | 1,109,064 | 1,996,019 | 210,034 | 100,816 | 2,995,869 | 2,318,553 | 347,167 | 1,819,827 | 421,552 | 1,052,954 |
| | 3 | 4,936,684 | 1,098,979 | 2,080,908 | 214,673 | 103,584 | 3,208,669 | 2,300,383 | 385,323 | 1,854,653 | 451,160 | 1,053,955 |
| | 4 | 7,858,218 | 1,131,055 | 2,170,783 | 229,706 | 117,720 | 2,896,249 | 2,346,262 | 389,420 | 1,831,986 | 444,789 | 1,017,550 |
| | | | | | | | | | | | | |
| 2017 | 1 | 7,232,707 | 1,118,373 | 2,067,899 | 223,828 | 97,295 | 3,204,078 | 2,338,463 | 374,854 | 1,914,669 | 451,530 | 1,046,358 |
| | 2 | 7,283,410 | 1,057,691 | 2,187,504 | 207,472 | 105,045 | 3,631,267 | 2,437,207 | 359,355 | 1,910,951 | 448,738 | 1,028,325 |
| | 3 | 5,137,218 | 1,144,597 | 2,365,766 | 222,983 | 113,969 | 3,198,026 | 2,434,184 | 395,146 | 1,982,315 | 459,599 | 998,075 |
| | 4 | 8,345,952 | 1,267,964 | 2,268,650 | 223,383 | 128,352 | 3,731,635 | 2,610,773 | 396,263 | 2,007,909 | 464,604 | 1,042,635 |
| | | | | | | | | | | | | |
| 2018 | 1 | 7,717,810 | 1,054,655 | 2,173,169 | 225,308 | 100,913 | 3,703,467 | 2,436,626 | 391,664 | 2,082,426 | 522,213 | 1,017,349 |
| | 2 | 7,716,375 | 1,129,287 | 2,259,893 | 221,254 | 111,470 | 3,846,566 | 2,528,958 | 383,333 | 2,169,733 | 506,999 | 1,004,546 |
| | 3 | 5,333,861 | 1,166,716 | 2,530,756 | 235,525 | 126,137 | 3,711,275 | 2,601,456 | 425,407 | 2,222,813 | 481,218 | 1,036,219 |
| | 4 | 8,736,201 | 1,308,537 | 2,659,683 | 246,088 | 138,991 | 4,394,440 | 2,829,714 | 403,987 | 2,261,589 | 479,286 | 1,036,859 |
| | | | | | | | | | | | | |
| 2019 | 1 | 8,139,275 | 1,159,804 | 2,280,570 | 249,013 | 108,984 | 4,201,084 | 2,529,025 | 390,255 | 2,312,794 | 563,309 | 1,069,349 |
| | 2 | 8,039,478 | 1,323,857 | 2,384,031 | 239,855 | 118,551 | 4,636,133 | 2,673,618 | 393,345 | 2,322,004 | 538,298 | 1,046,826 |
| | 3 | 5,485,725 | 1,413,025 | 2,749,036 | 247,875 | 139,826 | 4,350,024 | 2,794,017 | 442,538 | 2,407,844 | 516,819 | 1,084,998 |
| | 4 | 9,138,231 | 1,588,425 | 2,770,921 | 258,136 | 143,049 | 4,614,781 | 2,968,428 | 419,812 | 2,450,548 | 514,887 | 1,079,995 |
| | | | | | | | | | | | | |
| 2020 | 1 | 8,469,003 | 1,365,988 | 2,387,165 | 264,424 | 116,821 | 4,408,146 | 2,650,981 | 400,323 | 2,505,607 | 610,395 | 1,114,722 |
| | 2 | 8,366,922 | 1,438,625 | 2,479,030 | 247,858 | 124,044 | 5,203,762 | 2,668,493 | 330,902 | 2,541,456 | 592,499 | 1,078,981 |
| | 3 | 5,838,125 | 1,491,966 | 2,882,547 | 258,781 | 150,811 | 4,955,258 | 2,852,399 | 331,271 | 2,576,818 | 560,949 | 1,105,924 |
| | 4 | 9,649,835 | 1,590,872 | 2,897,536 | 278,547 | 148,483 | 4,854,506 | 3,024,946 | 357,157 | 2,669,394 | 549,186 | 1,113,341 |
| | | | | | | | | | | | | |
| 2021 | 1 | 8,694,642 | 1,489,458 | 2,532,535 | 283,588 | 127,311 | 4,641,094 | 2,768,552 | 374,418 | 2,730,301 | 661,347 | 1,144,304 |
| | 2 | 8,585,645 | 1,574,503 | 2,589,415 | 277,917 | 134,491 | 5,302,015 | 2,783,463 | 364,386 | 2,666,798 | 659,757 | 1,119,611 |
| | 3 | 6,140,943 | 1,677,259 | 2,995,394 | 284,691 | 157,663 | 5,241,139 | 2,905,381 | 378,526 | 2,560,195 | 607,521 | 1,158,549 |
| | 4 | 10,166,327 | 1,701,661 | 3,038,419 | 308,008 | 155,747 | 5,065,691 | 3,133,111 | 397,381 | 2,701,050 | 595,938 | 1,207,026 |
| | | | | | | | | | | | | |
| 2022 | 1 | 9,059,515 | 1,634,049 | 2,692,630 | 307,057 | 142,426 | 4,893,120 | 2,931,300 | 379,909 | 2,765,442 | 703,102 | 1,245,051 |
| | 2 | 8,858,422 | 1,665,101 | 2,711,874 | 302,142 | 147,326 | 5,512,600 | 2,918,632 | 411,599 | 2,775,195 | 704,239 | 1,220,918 |
| | 3 | 6,384,936 | 1,838,926 | 3,127,447 | 312,386 | 157,751 | 5,532,373 | 2,980,729 | 428,373 | 2,746,367 | 672,848 | 1,251,187 |
| | 4 | 10,408,404 | 2,008,066 | 3,092,193 | 320,547 | 159,251 | 5,192,938 | 3,215,788 | 431,217 | 2,774,947 | 632,221 | 1,306,985 |
| | | | | | | | | | | | | |
| 2023 | 1 | 9,384,414 | 1,865,624 | 2,865,062 | 331,948 | 149,709 | 5,151,185 | 3,106,347 | 426,514 | 2,829,232 | 748,368 | 1,416,306 |
| | 2 | 9,074,215 | 1,770,391 | 2,878,496 | 339,510 | 152,141 | 5,637,956 | 3,105,958 | 441,387 | 2,985,541 | 747,707 | 1,411,168 |
| | 3 | | | | | | | | | | | |
| | 4 | | | | | | | | | | | |

**Kiambatisho Na. 1 (Kinaendela.): Pato la Taifa kwa Shughuli za kiuchumi kwa Bei za Mwaka 2015 – Sh. Milioni**

| Mwaka | Nusu mwaka | Utawala na Ulinzi | Sughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundi | Huduma zinazohusiana na Utawala | Upangishaji Majengo | Elimu | Afya na Huduma za Jami | Huduma nyingine za Kijamii | Jumla ya Ongezeko la Thamani | Ongeza kodi katika bidhaa | Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2014 | | 4,242,164 | 447,921 | 1,976,260 | 2,828,970 | 2,186,260 | 1,349,941 | 1,088,317 | 80,873,021 | 8,001,090 | 88,874,111 |
| 2015 | | 4,548,604 | 518,123 | 2,183,917 | 2,949,598 | 2,413,306 | 1,419,090 | 1,144,099 | 86,484,736 | 7,864,579 | 94,349,316 |
| 2016 | | 4,793,820 | 606,207 | 2,611,498 | 3,077,086 | 2,665,336 | 1,497,896 | 1,278,046 | 92,803,857 | 8,024,535 | 100,828,393 |
| 2017 | | 4,907,113 | 694,291 | 2,892,463 | 3,211,895 | 2,859,171 | 1,611,999 | 1,409,504 | 99,253,451 | 8,393,240 | 107,646,691 |
| 2018 | | 5,064,968 | 763,332 | 3,054,288 | 3,354,518 | 3,046,789 | 1,746,731 | 1,516,831 | 106,218,226 | 8,923,222 | 115,141,448 |
| 2019 | | 5,238,491 | 821,636 | 3,311,753 | 3,505,485 | 3,257,406 | 1,833,514 | 1,627,511 | 113,894,194 | 9,303,276 | 123,197,471 |
| 2020 | | 5,438,146 | 881,833 | 3,569,800 | 3,663,972 | 3,365,355 | 1,953,479 | 1,668,877 | 120,046,265 | 9,093,542 | 129,139,806 |
| 2021 | | 5,714,547 | 942,013 | 3,817,047 | 3,827,460 | 3,538,281 | 2,065,677 | 1,840,290 | 125,828,485 | 9,693,238 | 135,521,723 |
| 2022 | | 6,024,203 | 996,609 | 3,993,799 | 3,997,460 | 3,724,729 | 2,176,986 | 1,998,754 | 131,870,070 | 10,002,660 | 141,872,730 |
| | | | | | | | | | | | |
| 2012 | 1 | 803,642 | 74,831 | 340,487 | 641,698 | 461,652 | 309,228 | 217,530 | 17,788,914 | 1,732,167 | 19,521,081 |
| | 2 | 817,057 | 78,603 | 347,905 | 648,276 | 447,191 | 320,506 | 221,443 | 17,276,676 | 1,596,603 | 18,873,279 |
| | 3 | 976,077 | 82,451 | 358,076 | 654,899 | 505,099 | 339,618 | 234,892 | 16,641,764 | 1,737,034 | 18,378,797 |
| | 4 | 1,026,348 | 86,375 | 371,000 | 661,566 | 508,702 | 315,242 | 236,523 | 19,310,723 | 1,895,967 | 21,206,689 |
| 2013 | 1 | 897,436 | 90,376 | 386,679 | 668,325 | 454,979 | 299,454 | 239,370 | 18,443,971 | 1,947,582 | 20,391,553 |
| | 2 | 945,222 | 94,335 | 404,378 | 675,175 | 462,904 | 314,552 | 240,745 | 18,180,405 | 1,975,657 | 20,156,062 |
| | 3 | 1,061,729 | 98,252 | 424,098 | 682,119 | 501,425 | 323,848 | 253,497 | 17,755,599 | 2,088,269 | 19,843,868 |
| | 4 | 1,069,818 | 102,128 | 445,840 | 689,157 | 508,325 | 307,176 | 257,849 | 20,709,012 | 2,167,622 | 22,876,634 |
| | | | | | | | | | | | |
| 2014 | 1 | 1,007,519 | 105,963 | 469,602 | 696,292 | 510,028 | 322,658 | 266,230 | 20,026,099 | 2,102,819 | 22,128,918 |
| | 2 | 1,022,325 | 109,904 | 488,892 | 703,526 | 525,815 | 342,267 | 268,409 | 20,039,997 | 1,866,580 | 21,906,577 |
| | 3 | 1,105,719 | 113,951 | 503,710 | 710,859 | 571,648 | 346,149 | 276,932 | 18,794,219 | 1,989,729 | 20,783,948 |
| | 4 | 1,106,601 | 118,104 | 514,055 | 718,293 | 578,769 | 338,867 | 276,745 | 22,012,706 | 2,041,962 | 24,054,668 |
| | | | | | | | | | | | |
| 2015 | 1 | 1,033,818 | 122,364 | 519,928 | 725,830 | 557,686 | 331,321 | 277,986 | 21,056,161 | 1,721,421 | 22,777,583 |
| | 2 | 1,067,508 | 126,934 | 532,698 | 733,472 | 573,927 | 344,848 | 279,553 | 21,414,740 | 1,952,108 | 23,366,848 |
| | 3 | 1,227,874 | 131,816 | 552,364 | 741,220 | 640,405 | 377,131 | 291,033 | 20,228,053 | 2,137,973 | 22,366,026 |
| | 4 | 1,219,405 | 137,009 | 578,927 | 749,076 | 641,287 | 365,789 | 295,528 | 23,785,782 | 2,053,077 | 25,838,859 |
| | | | | | | | | | | | |
| 2016 | 1 | 1,236,354 | 142,513 | 612,386 | 757,042 | 672,749 | 383,295 | 303,604 | 23,034,254 | 1,945,089 | 24,979,343 |
| | 2 | 1,233,036 | 148,330 | 641,965 | 765,119 | 676,794 | 383,518 | 309,726 | 23,383,437 | 1,904,859 | 25,288,296 |
| | 3 | 1,152,150 | 154,460 | 667,664 | 773,310 | 651,053 | 361,396 | 326,868 | 21,775,874 | 2,059,788 | 23,835,662 |
| | 4 | 1,172,280 | 160,904 | 689,482 | 781,616 | 664,740 | 369,687 | 337,848 | 24,610,293 | 2,114,799 | 26,725,092 |
| | | | | | | | | | | | |
| 2017 | 1 | 1,170,421 | 165,581 | 702,756 | 790,039 | 683,657 | 384,401 | 340,985 | 24,307,893 | 1,900,901 | 26,208,794 |
| | 2 | 1,240,920 | 170,998 | 716,993 | 798,581 | 716,737 | 410,459 | 344,490 | 25,056,143 | 1,922,024 | 26,978,167 |
| | 3 | 1,238,527 | 176,281 | 730,234 | 807,244 | 724,292 | 401,401 | 358,976 | 22,888,834 | 2,145,352 | 25,034,185 |
| | 4 | 1,257,246 | 181,430 | 742,480 | 816,031 | 734,485 | 415,738 | 365,053 | 27,000,581 | 2,424,964 | 29,425,545 |
| | | | | | | | | | | | |
